Katika mfano huu, kina –***ye*** kinapatikana katika utungo mzima wa *Inkishafi.* Mtindo huu unatumika katika karibu tenzi zote za jadi. *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa (kina –**ya**), Utenzi wa Fumo Liyongo* (Kina-***ya)*** n.k. Hata hivyo, ingawa tenzi za jadi zilikidhi mahitaji ya mizani nane, baadhi yazo zilipungukiwa katika kuzingatia kina kimoja katika utungo mzima. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Masahibu,* baadhi ya beti zina kina ***–a*** na nyingine –***ya***, *Utendi wa Mwana Kupona* una baadhi ya beti zenye kina –***ya***, nyingine –***a*** na –***wa***.

Watunzi wa baada ya kina *Mwana Kupona* walijaribu pia kutilia maanani mizani na vina katika tungo zao. Kwa mfano Muhammad Kijumwa katika *Utendi wa Siraji* anatumia kina *-**a*** katika karibu beti zote isipokuwa ni tofauti katika baadhi ya beti kama vile ubeti wa 123 na 165 kuna kina ***–ya.*** Hata Shaaban Robert anajaribu kuzingatia vina katika *Utenzi wa Hati* na *Utenzi wa Adili* ingawa kuna upungufu wa ulinganifu.

Nabhany (1987)[1] anadai kuwa tenzi siku zote hutumiwa kwa kusimulia hadithi za pahala au za watu ambao ni mashujaa na maarufu. Vilevile hutumiwa kwa kutolea waadhi au Wosia. Yote haya ni kwa sababu tenzi ndiyo bahari ya pekee katika ushairi wa Kiswahili iwezayo kuelezea jambo kwa urefu sana bila ya kumchokesha mtu. Maelezo haya ya Nabhany yanapata mifano kutoka *Inkishafi* (unahusu ufanifu na uvunjifu wa Wafalme na Mji wa Pate), *Utenzi wa Mwana Kupona* (unahusu wosia wa Mwana Kupona kwa bintiye Mwana Hashima binti Mataka), *Utenzi wa Fumo Liyongo* ( unamhusu shujaa wa Uswahilini Fumo Liyongo) n.k.

**Mashairi**

Baada ya enzi ya tenzi kukawa na *mashairi.* Shairi hutumiwa kwa kufumba, kuichezea lugha kwa ujuzi na uhodari, kuhifadhia maneno mazito na magumu na vilevile katika mashindano na mapambano ya washairi (Nabhany 1987). Naye Shitemi (2010) anasema kuwa Shairi huzungumzia mada maalum yenye kurejelewa na kusisitizwa katika kila ubeti. Mara nyingi hutumia lugha nzito yenye kuelezea hisia za ndani kwa njia yenye kugusa nathari za msikilizaji kwa njia ya kipekee. Mashairi yalishika mizizi katika Karne ya 19 kupitia mshairi mtajika Muyaka bin Haji (1776-1840). Mashairi yake ni ya kitarbia, yenye mishororo minne minne katika kila ubeti, kina cha kati na cha nje, mizani nane; na kibwagizo ama cha mkarara au kisichokuwa cha mkarara mwishoni mwa kila ubeti. Kwa mfano:

Oa kwamba U muozi, uzoeleo kuowa
Oa mato maolezi, na mboni ukizikowa
Oa maji maundazi, meupe kama maziwa
Oa sizi ndizo ndowa, asokuoa ni yupi ?

Oa ndiwe muolezi, uzoeleo kuowa
Oa sifumbe maozi, maninga uchiyavua
Oa uzaze uzazi, kama ulivyozaliwa
Oa sizi ndizi ndowa, asokuoa ni yupi?
(…) (*Shitemi 2010:101*)

Mfano huu ni shairi lenye mishororo minne kila ubeti, vipande viwili, vina vya kati na mwisho na kibwagizo chenye mkarara. Hata hivyo, mashairi hutofautiana katika vina na mipangilio ya mishororo na vipande vya mishororo. Tofauti hizi zinazua bahari nyingine katika ushairi wa Kiswahili kama vile *tathnia, takhmisa, mtiririko, ukara, mathnawi, utenzi, ukawafi na mavue.* Huweza kutofautiana pia kwa upande wa mizani ambapo tunapata bahari kama vile *mkufu, kikwamba* n.k. Cha msingi na muhimu ni kwamba shairi ni utungo mfupi ukilinganishwa na tenzi, kwa mfano mashairi ya Shaaban Robert katika *Pambo la Lugha* (1966) ni ya ubeti mmoja mmoja, beti mbili mbili, tatu tatu, nne nne n.k

Abdulaziz (1979) anasema kuwa bila shaka Muyaka ni kielelezo cha upeo wa mabadiliko na maendeleo ya ushairi maarufu wa Kiswahili. Washairi baada yake walioandika kwa umbo la mashairi wanaonekana waliathiriwa na mtindo wake wa uteuzi na matumizi ya maneno. Hali hii ni ukweli hasa kwa Ahmed Nasser Juma Bhalo. Marehemu Shaaban Robert, mshairi mwingine maarufu wa Karne ya 20 kutoka Tanzania anadhihirisha kwa kiasi fulani athari za kimtindo ambazo zinaweza kuhusishwa na Muyaka. Maelezo haya ya Abdulaziz (1979) yanaashiria kuwa Shaaban Robert aliuendeleza mtindo wa mashairi ya Muyaka. Kwa mfano shairi *Dunia:*

(…)
Ajae ardhi hii, kutoka katika mimba
Mizizini au yai, au katika kitamba
Milki hakinai, ya mali wala mashamba

[1] Maelezo ya Ahmed Nabhany katika *Utangulizi* wa *Malenga wa Karne Moja* (1987) – S. Chiraghdin.

Mwisho wa uhai, kaburi lake jembamba
(…)
Mtu hashibi pato, hili huonyesha nini?
Laonyesha kama pito, kuwa yumo safarini
Enda kuitika wito, bora usio kifani
Ambao kila mtoto, wa Adamu hutamani

Yumo katika safari, kila mwanadamu
Haraka au usiri, kwenda imelazimu
Epusha roho kahari, yake na jahanamu
Iwe katika safari, mwili ukiwa kuzimu
(*Pambo la Lugha, 8*)

Shaaban Robert, Kama Muyaka katika shairi *Dunia Mti Mkavu* (katika Abdulaziz 1979:63), anatuchorea uvunjifu wa dunia katika shairi lenye umbo la kitarbia. Purukushani za binadamu huwa na mwisho wake. Robert anazungumzia kuhusu "*Kaburi Jembamba*" ilhali Muyaka anasema "*Kurudi nyuma si kazi*" kuashiria hatma ya binadamu.
Mwingine anayeonekana kuathiriwa na mashairi ya Muyaka ni Kaluta Amri Abedi. Anatumia takriri neno katika shairi *Oa Mwanakwetu Oa;*

(…)
Oa mke kufu yako, mnayefanana hali
Oa wa kikozi chako, wa asili na fasili
Oa binti ami yako, ikuwiapo sabali
Oa, muovu sioe, Oa mwanakwetu oa

Oa mrembo wa shari, mwenye hadhi na murua
Oa mwema na watani, uwezapo mgundua
Oa, sioe muhuni, moto umejipalia
Oa, muovu sioe, Oa mwanakwetu oa
(…) (*Abedi 1954:29*)

Msisitizo unaotokana na neno ***oa*** katika shairi la Abedi una athari sawa na ule unaopatikana katika shairi ***oa*** la Muyaka ambalo tayari tumeliangazia hapo awali.

**Mashairi Huru**
Katika historia ya ushairi wa Kiswahili, mashairi huru ni utanzu unaohusishwa na wale waliopata kisomo cha chuo kikuu katika miaka ya 1960 nchini Tanzania. Abdulaziz (1979) anasema kuwa watunzi hawa wapya walipata elimu ya chuo kikuu na wakatagusana kwa kiasi kikubwa na kazi za kifasihi kutoka tamaduni nyingine. Hawa ni Euphrase Kezilahabi na Ebrahim Hussein, wote wakiwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam mnamo 1968/1969.

Indede (2008) anahoji kuwa utangamano katika mifumo mbalimbali ya kielimu ni shughuli ambayo imechangia sana mabadiliko ya umbo la ushairi. Ni kweli kwamba utangamano kati ya wasomi wa Kiafrika na watu wa mataifa mbalimbali ikiwemo Marekani, Uingereza, Ujerumani, umeandaa mawazo, fikra, mazingira na mawanda mageni katika fani hii. Changamoto na utangamano huu wa kilimwengu kumewafanya washairi huru kuamua kubadilisha miundo na mitindo ya mitazamo ya kifasihi. Hii ndiyo sababu tunapata kwamba mielekeo ya kifasihi ya kipindi baada ya uhuru ilivunja umbo la kitamaduni na kufanyia majaribio maumbo mapya ya ushairi. Mtagusano anaouzungumzia Indede (2008) ni ule uliowafanya watunzi hawa wapya kukiuka kaida zilizozoeleka katika ushairi wa arudhi. Walivunja kaida zilizoshikiliwa na kina Muyaka bin Haji na Kaluta Amri Abedi. Kwa mfano shairi la Kezilahabi, *Kisu Mkononi:*

Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
Siwezi, kama gurudumu nitajiviringisha.
Mtelemko mkali huu.
Lini na wapi mwisho sijui

Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu ya dhambi.
Kisu ! Maisha kafiri haya

Kama kutazama nyuma au mbele
Ni kufa moyo mzima!

Sasa kama Simba-mtu shauri nimekata.
Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili.
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,
Kila mpigo wa moyo wangu
Huu mpigo muziki wa maisha.[2]

Mfano mwingine ni wa Ebrahim Hussein, *Ngoma na Vailini:*

Huo, huo, mpwitompwito wa ngoma
Unachemsha damu yangu na matamanio yaliyo ladha

Damu iliyopozwa na kubembelezwa
Na vailini nyororo, vailini inayonita
Kwa huzuni yenye furaha

Sasa nacheka na kupwitapwita
Sasa na furaha na kuburudika
Mdundo wa maisha
Raha ya nafsi
Wapi niende?

Lazima niswali, lazima niabudu
Nimuabudu Allah
Lakini ataisikia sauti yenye panda
Sauti inayotokana na mwenye kuvaa
Kanzu na msalaba?

Mashairi haya mawili hayajazingatia kanuni ya vina na mizani wala ulinganifu wa idadi ya mishororo. Yametumia rasilmali za kiisimu kupitisha jumbe nzito kuhusu maisha ya binadamu. Kwao, kilicho muhimu ni yaliyomo, si vina na mizani. Muhimu ni namna lugha inavyotumiwa kisanii ili kumtafakarisha na kugusa hisi za ndani za msomaji au msikilizaji. Kwa jumla, mashairi huru yamechangia katika kuibuka kwa maumbo na mitindo mipya kama ilivyo katika kazi za watunzi kama vile Alamin Mazrui aliyechapisha diwani *Chembe cha Moyo* (1988). Yamechangia pakubwa katika kupanua peo za ushairi wa kimajaribio.

**Mashairi Picha**

Ushairi wa kimajaribio ni ule ambao tunaweza kuuhusisha zaidi na mshairi wa Kenya, Kithaka wa Mberia.[3] Diwani zake ni kama vile *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine (*2001), *Redio na Mwezi* (2005) na *Msimu wa Tisa* (2007). Mberia anajitosa katika majaribio ya lugha katika kiwango cha umbo. Kwa mfano, katika shairi *Amba*, Mberia ametumia kina -*mba* ili kusuka matini (Bertoncini 2010, Frolova 2007):

(…)
Natangaza kwamba
Huyu mamba
Ndiye mwamba
Unaoharibu shamba

Bali naamba
Ingawa amejipamba
Kwa magamba
Hatashinda kamba

[2] Limenukuliwa kutoka kwa Abdulaziz (1979), *uk 103-104.*

[3] Kithaka wa Mberia ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Licha ya kutunga mashairi, ametunga pia tamthilia kama vile *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (2001).

Ivunjayo miamba
Kwenye mashamba
*(Mberia 1997)*

Majaribio mengine anayoyafanya Mberia ni kurudia mashina ya maneno ili shairi liwe na tuni spesheli:

Ewe bara Jipya
Nyota unayomwesamwesa
Katika majira ya gizagiza
Nyota unayemetameta
Kama uhai unaopwitapwita
(…) (*Mberia 2001*)

Licha ya majaribio haya ya kiisimu, Mberia amefanya majaribio ya kiumbo na kuibuka na mashairi picha. Umbo la kipekee limejitokeza ambalo linamwezesha msomaji kuona kile kinachowasilishwa na mshairi. Kwa mfano, katika shairi *Nyumba*, tunaweza kuona mchoro wa nyumba ambayo inawakilisha nchi inayojengwa na watu masikini lakini hawafaidi kutokana na ujenzi huu;

Nyumba
hii ambayo
ilifumbwa kwa
mawe yaliyoumbwa
na maumbile,
mawe ambayo
yalisongwa na
masikini nyumba
hii ambayo
ilisimamishwa kwa
saruji itokanayo
na viungo
vya ardhi vilivyochimbwa na
yahe, nyumba
hii iliyoezekwa
vigae vitokanavyo
na udongo
kimano tuliourithi kutoka mama, nyumba
hii

Iliyopambwa kwa vioo vilivyotengenezwa na
matambara, kwa nini wasistarehe katika nyumba
hii wale amabo misuli yao iliipa uhai?
*(Mberia 1997)*

Mfano mwingine ni shairi *Boga* linalochukua umbo la Kabeji ambayo imekomaa. Katika ushairi wa Kiswahili sasa tuna maumbo kama vile duara, nusu duara, umbo la ramani ya Afrika n.k. Ushairi huru basi umepelekea kuchipuka kwa maumbo na mitindo mbalimbali katika ushairi wa Kiswahili. Ni mabadiliko yanayoweka tarehe mpya katika historia na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, matini za kishairi zinapata sura mpya kadri jamii inavyopiga hatua kiteknolojia katika enzi hii ya utandawazi.

**Hitimisho**

Makala hii imedhihirisha kuwa ukiushi wa kaida za kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili umechangia katika kurutubisha na kupanua taaluma hii. Haya yanatokana na juhudi za watunzi za kuwania kuibuka na maumbo pamoja na mitindo mipya ya kiutunzi. Juhudi hizi zinaupa ushairi wa Kiswahili uhai mpya unaosaidia katika makuzi ya utanzu huu. Hata hivyo, kaida za kiutunzi bado zinachukua nafasi kubwa zaidi hata katika ushairi wa kisasa. Hii ni kwa sababu kaida hizi huibua miundo na maumbo yaliyo na upekee wa kiujumi na kiumbuji. Kwa jumla, ku(to)kiukwa kwa kaida za kiutunzi kunasaidia katika kupanua peo na mawanda ya ushairi wa Kiswahili.

**Marejeleo**

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: KLB.
Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: KLB.
Bertoncini, E. Z. (2010). *Some Remarks on Kithaka wa Mberia's Poetry. SWAHILI FORUM* 17 (2010) *uk 91-103*.
Coulthard, M. (1985). *An Introduction to Discourse Analysis*, 2nd Ed. Harlow: Longman.

Frolova, N. (2007). *The 'Renovated' Poetry of Theobald Mvungi and Said Ahmed Mohamed: On Mechanisms of Transformation of Traditional Swahili Verse. SWAHILI FORUM* 14 (2007) *uk 5-15*.

Indede, F. (2008). *Mabadiliko katka Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi wa Kiswahili. SWAHILI FORUM* 15 (2008) *uk 73-94*.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.

Mlamali, M. (1981). *Inkishafi: Ikisiri ya Muhamadi wa Mlamali*. Nairobi: Longman.

Robert, S. (1966). *Pambo la lugha*. Nairobi: Oxford Universty Press.

Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.

Wamitila, K. W. (2006). *Kamusi ya Ushairi*. Nairobi: Vide-Muwa.

_____________(2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.